Tanzania Human Rights Defenders Coalition
[THRDC]
P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail; info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

TAMKO KUHUSU KULEGEZA GHARAMA ZA MATUMIZI YA TEHAMA NA INTANETI KATIKA KIPINDI HIKI CHA CORONA (COVID-19)

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unapenda kuchukua fursa hii kuwasilisha maombi yetu kwa kampuni za mitandao ya simu, watoa huduma za intaneti na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuhusu kupunguza gharama za huduma na bidhaa zao kwa wateja katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID-19) hapa nchini.

Kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Corona (COVID-19) nchini tangu tarehe 16 Machi 2020, ambapo serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitangaza kisa cha kuwepo kwa mgonjwa wa kwanza wa Corona Tanzania, na baadaye kuilazimu serikali kufunga shule, vyuo vikuu na kuweka katazo la mikusanyiko isiyo ya lazima, vivyo hivyo katika kipindi cha hivi karibuni biashara nyingi na ofisi mbalimbali zimelazimika kufunga ofisi zao kwa hofu ya kusambaa kwa ugonjwa huu miongoni mwa wanajamii. Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, hadi kufikia jana tarehe 28 Aprili 2020, idadi ya visa vya wagonjwa wa corona nchini vilikuwa 480, huku waliopona ni 167 na waliofariki dunia wakiwa 16.

Kwa hali ya sasa, ni dhahiri kwamba, wanafunzi, walimu, wafanyabiashara, watetezi wa haki za binadamu, wafanyakazi wa AZAKi zilizofunga ofisi zao pamoja na familia nyingi zimelazimika kukaa na kufanyia shughuli zao majumbani. Bila shaka, hali hii imeziongezea faida maradufu kampuni za mitandao ya simu, kampuni za huduma ya intaneti na kampuni za huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa kuwa vifaa vya mawasiliano kama vile simu na kompyuta ndio njia mbadala za mawasiliano kwenye jamii na hata ulimwenguni katika kipindi hiki cha janga la Corona.

Kwa kutumia mifano ya nchi kama vile Marekani na Uingereza ambako maambukizi ya Corona yameshamiri kwa sasa na kupelekea serikali za nchi hizo kuweka makatazo ya wananchi kutoka nje ya nyumba zao, kampuni za mitandao ya simu pamoja na kampuni za watoa huduma za intaneti kwenye nchi hizo kama vile AT&T na Comcast za Marekani na Virgin Media na Vodafone za Uingereza na zingine nyingi zimepunguza bei za huduma zao kwa wateja wao. Watoa huduma wengine wamekwenda mbali zaidi na kutoa huduma za intaneti bure kwa kipindi cha miezi miwili au zaidi.

Hivyo basi, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unapenda kuchukua nafasi hii kuwaomba watoa huduma ya intaneti, kampuni za mitandao ya simu, kampuni za huduma za TEHAMA, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), watetezi wa haki za binadamu, wana-AZAKi, Serikali na watumiaji wa huduma hizi kuchukua hatua zifuatazo;

WITO WETU:

1) Tunawashauri watetezi wa haki za binadamu pamoja na wana-AZAKi wawe mfano wa kuigwa na jamii kwa kutumia mitandao ya mawasiliano kufanya shughuli zao majumbani. Programu rahisi na salama kwa mikutano ya mitandaoni ni kama Zoom.com, Jitsi Meet, BlueJeans, Wire na Skype. Programu salama kwa jumbe fupi au kuchati ni WhatsApp, Signal na Telegram.

2) Tunaomba kampuni za mitandao ya simu, watoa huduma za intaneti pamoja na wauzaji wa bidhaa za TEHAMA kupunguza gharama za huduma na bidhaa zao na kuwa wabunifu kwa kutoa bando zenye bei nafuu kwa kiasi fulani ili watanzania waweze kupata unafuu wa huduma za mawasiliano kipindi hiki ambacho wanafanyia kazi zao majumbani na wanafunzi wanatumia intaneti kwa ajili ya kujifunza.

3) Pia tunaomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itoe agizo kwa kampuni za mitandao ya simu na watoa huduma ya intaneti kupunguza gharama za huduma zao au kutoa baadhi ya huduma zao bure kama vile Wi-Fi za bure kwenye maeneo kama vituo vya mabasi.

4) Huu ni muda muafaka kwa TCRA pia kupunguza au/na kuondoa kabisa gharama za usajili wa mitandao kama vile YouTube na Blogu ili walimu waweze kuitumia kuwafundishia wanafunzi na hata wananchi kuitumia kuelimishana miongoni mwao.

5) Tunawashauri wanafunzi kutulia majumbani mwao na kutumia mitandao ya kijamii pamoja na televisheni za elimu kujielimisha zaidi na si kuzitumia vibaya.

6) Wauzaji wa bidhaa za TEHAMA kama vile simu na kompyuta wanapaswa kupunguza gharama za bidhaa zao ili kuwapa unafuu wateja wao kwa kuzingatia kuwa hali ya kiuchumi kwa familia nyingi katika kipindi hiki cha Corona si nzuri.

7) Tunawaomba watumiaji wa mitandao ya simu, watumiaji wa intaneti, watumiaji wa vifaa vya kidijitali kama simu na kompyuta na umma kwa ujumla kujikinga na wahalifu, matapeli na wadukuzi mitandaoni, na kuendelea kudumisha mawasiliano ya mbali bila kukusanyika kuepuka maambukizi ya Corona.

8) Pia tunawashauri watumiaji wa huduma za intaneti pamoja na huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia mitandao ya simu na benki kutumia vema rasilimali fedha walizonazo kwa sasa na kuzingatia kuweka akiba ya baadaye kwani haijulikani janga hili litaisha lini.

9) Tunaishauri Wizara ya Fedha kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupunguza kodi ya huduma za intaneti kwa watoa huduma, ili watanzania wanufaike na matumizi ya intaneti katika kipindi hiki.

10) Tunawashauri wafanyabiashara nao waitumie vizuri mitandao kufanya mauzo ya bidhaa au huduma zao ili kupunguza misongamano isiyokuwa ya lazima madukani.

11) Tunalisihi Jeshi la Polisi lisiwakamate watanzania wanaotumia uhuru na haki yao ya kupashana habari mitandaoni katika kipindi hiki, badala yake jeshi la polisi liendelea kuwalinda watumiaji wa mitandao dhidi ya wahalifu wanaotumia mwanya wa janga hili la Corona kufanya uhalifu mitandaoni.

12) Kwa kutambua mchango mkubwa wa Mkongo wa Taifa katika kusambaza huduma ya intaneti nchini na hata nchi jirani, tunaiomba mamlaka husika inayosimamia Mkongo wa Taifa, ihakikishe makampuni ya mitandao ya simu ndani na nje ya Tanzania pamoja na watumiaji wa huduma ya intaneti wanaendelea kupata intaneti ya kasi na yenye ubora katika kipindi hiki.

13) Mwisho kabisa, tunaiomba Serikali, Wizara ya Elimu na Wazazi wenye wanafunzi, waweke utaratibu wa kuwawezesha walimu kifedha ili waendelee kufundisha kupitia mitandao, kwani walimu nao wana mahitaji yao kama walivyo wanataaluma wengine.

Imetolewa na:

Onesmo Olengurumwa,
Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC),
Tarehe 29 Aprili 2020

Board of Directors:
Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.
Defending Human Rights is not a Crime!